

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
28 Machi 2009**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Athumani Mussa
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Edgar R Paulo
Edward Marline
Elaine Baker
Filbert Mbecha
George Kabogo
Hamadi Hatibu Bwaja
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Ayuba
Kibwana Mohammad Msiga
Mejah Mbuya
Mohammed Samwely
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Saidi Brashi
Selion Elieskia
Shamte J Kigoma

Kongamano

Elaine aliwasiliana na email na Benki ya Dunia (World Bank) na ubalozi wa Uholonzi kuomba walipe posho kwa kongamano lakini wote wamekataa. Ubalozzi wa Uholonzi bado wapo tayari kuchangia ukumbi na vinyaji.

Edgar alipeleka barua JICA kuomba tukutane nao. Mtu anayehusika alikuwepo kwenye mkutano mwingine. Atafuatalia tena wiki hii.

Mradi wa Wamba

Una Osili bado hajatumia documents kuonyesha NMB kwamba transfer ilikuwa transferred. Elaine atafuatalia kwa email.

Ruzuku ya Foundation for Civil Society Grant

Elaine anafuatalia kupata CVs za waalimu wa kompyuta.

Fasta cycle couriers

Edgar alipeleka barua ofisa ya ushirika Kinondoni. Ofisa alimpigia simu Mejah kusema kwamba barua ipigwe mihuri ya serikali ya mtaa na ya kata kwanza. Mejah na Juma watafuatalia kupata mihuri.

Video ya usalama wa baisikeli

Elaine atatengeneza DVDs na CDs. Mwanachama mpya Edward Martin alisema atasaidia kutengeneza video nyingine ya UWABA.

Mashindano ya wimbo

Mejah na Edgar walipata taarifa kwamba kutengeza single ina gharama ya Tsh 150,000 kutoka kampuni kama 41 records. Tulikubali kumwalika Elia kwenye mkutano ujao kuimba wimbo wa baisikeli.

Mkutano wa WHO

WHO (shirika la afya la dunia) wamejibu kwamba wanaweza kutoa fedha kwa mtu mmoja kutoka UWABA kuhudhuria mkutano wa usalama barabarani. Kama tulivyokubali wiki jana, Elaine alijaza fomu kwa ajili ya Mejah. Atafuatalia kupata barua ya mwaliko inayo jina la Mejah ili apate visa.

Re-cycle

Re-cycle walitutumia email kusema kuna mtu yupo tayari kuchangia gharama za usafiri wa baisikeli kutoka UK mpaka Dar es Salaam, lakini siyo gharama zote. Tulikubali kuandika barua kwa TRA kuomba samehe ya kodi. Mejah na Kibwana pia watatafuta taarifa zaidi kuhusu vipi kupata samehe.

Kiingereza

Athmani Mussa ni mwalimu wa kiingereza na yupo tayari kuchangia muda kufundisha wanachama wa UWABA kiingereza kila siku saa saba kwa masaa mawili. Wanachama walijiandikisha kwa mafunzo. Elaine alisema kabla mkutano unapoanza, wanaowahi wanaweza kuongeana kiingereza ili kupata mazoezi. Mikutano bado itakuwa kwa Kiswahili kwa sababu kuna wanachama wengine hawajui kiingereza.

Hela na guta

Ramadhan alilipa Tsh 14,000 ya hela ya guta na bado anadaiwa Tsh 7,000. Juma ana Tsh 21,000 ya hela ya UWABA.